**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Mchango wa Kiswahili katika Mofofonolojia ya Nominomkopo za Lubukusu

*Tom Juma James[1*] na Dkt. Jacktone Onyango, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100 Nairobi, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: tomjames558@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*06 Aprili 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Mofofonolojia, Lubukusu, Mlingano Chanzi, Usimilisho, Lugha Chanzi, Lugha Pokezi, Ukopaji.*

**IKISIRI**

Ukopaji wa leksimu baina ya lugha tofauti ni jambo ambalo haliwezi kuepukika. Kwa hivyo, makala haya yamechunguza jinsi lugha ya Kiswahili imechangia katika upanuzi wa Lubukusu kimofofonolojia kupitia ukopaji wa nomino. Hali hii ilisababishwa na dhana kwamba Kiswahili kimeathiri Lubukusu kiisimu kupitia vipengele kama vile fonolojia, mofolojia na sintaksia. Hata hivyo,makala haya yamejikita tu katika viwango viwili vya kiisimu; fonolojia na mofolojia. Malengo matatu yalishughulikiwa katika makala haya ambayo ni: kubainisha mabadiliko ya kifonolojia yaliyojitokeza katika nominomkopo kutoka Kiswahili hadi Lubukusu, kutambulisha mabadiliko ya kimofolojia yaliyojitokeza katika nominomkopo kutoka Kiswahili hadi Lubukusu na kuchunguza ulinganifu wa kifonolojia na kimofolojia uliopo baina ya nominomkopo za Lubukusu na leksimu changizi za Kiswahili. Hatua zote za makala haya zilitimizwa kupitia mihimili ya nadharia ya Mlingano Chanzi, modeli ya kiutohozi iliyoasisiwa na Smith (2009) na ni maendelezo ya Nadharia Upeo (*OptimalityTheory*) iliyopendekezwa na Prince na Smolensky (1993). Data ilikusanywa kutoka maktabani na nyanjani. Data ya maktabani ilipatikana kupitia udurusu wa vitabu, tasnifu, majarida na makala ya mtandaoni. Nyanjani, sampuli iliteuliwa kimaksudi kupitia mahojiano kwa walengwa 24 wa jamiilugha ya Babukusu kutoka Kaunti Ndogo ya Kiminini, Kauntiya Trans-Nzoia. Mahojiano yalihusu habari za kibinafsi na maswali teule kutoka kwa vikoa 12 vya kisemantiki. Uchanganuzi wa nominomkopo zilizokusanywa kutoka nyanjani ulidhihirisha kwamba kuna mfanano wa kimaumbo kati ya nomino hizo zikiwa katika mazingiraya Kiswahili na hata zinapohamishiwa katika mazingira ya Lubukusu. Uchunguzi wa matokeo ulionyesha kwamba nominokopwa za Lubukusu kutoka Kiswahili hupitia mabadiliko ya kifonolojia, kimofolojia na mabadiliko hayo yaliongozwa na sheria za

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

kimofofonolojia zilizorahisisha usimilisho wa nomino hizo kopwa katika sarufi ya Lubukusu.

**APA CITATION**

James, T. J. & Onyango, J. (2023). Mchango wa Kiswahili katika Mofofonolojia ya Nominomkopo za Lubukusu *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 49-67. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162.

**CHICAGO CITATION**

James, Tom Juma and Jacktone Onyango. 2023. "Mchango wa Kiswahili katika Mofofonolojia ya Nominomkopo za Lubukusu". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 49-67. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162.

**HARVARD CITATION**

James, T. J. & Onyango, J. (2023) "Mchango wa Kiswahili katika Mofofonolojia ya Nominomkopo za Lubukusu", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 49-67. doi: 10.37284/jammk.6.1.1162.

**IEEE CITATION**

T. J. James & J. Onyango, "Mchango wa Kiswahili katika Mofofonolojia ya Nominomkopo za Lubukusu", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 49-67, Apr. 2023.

**MLA CITATION**

James, Tom Juma & Jacktone Onyango. "Mchango wa Kiswahili katika Mofofonolojia ya Nominomkopo za Lubukusu". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Apr. 2023, pp. 49-67, doi:10.37284/jammk.6.1.1162.

## UTANGULIZI

Makala haya yamechunguzaathari za mtagusano waKiswahili na Lubukusu kimofofonolojia kupitia ukopaji wa nomino kutoka Kiswahili hadi Lubukusu. Ukopaji ni uhamishaji wa sauti, leksimu, msamiati au maneno kutoka lugha moja hadi nyingine (Mesthrie na wenzake, 2000).Ukopaji wa nomino kutoka Kiswahili hadi Lubukusu umehakikiwa kupitia ulinganisho na ulinganuzi wa vipengele mahsusi wa fonolojia na mofolojia kwa sababu Wohlgemuth (2009) anaeleza kwamba mtafiti anayeazimia kutathmini ulinganifu wa kileksimu uliopo baina ya lugha mbili, ni lazima achunguzemanenokopwa baina ya lugha hizo. Ni kutokana na mazingara haya ya mtagusano wa lugha ndiposa Kiswahili kimeathiri Lubukusu kimofofonolojia kupitia ukopaji wa nomino. Mofofonolojia ni tawi la isimu linalochunguza uhusiano uliopo baina ya fonolojia na mofolojia (Massamba, 2009: 54; Karanja & Habwe, 2004). Iribemwangi na wenzake (2013: 57) wanasisitiza kuwa tawi la mofofonolojia halijapewa kipaumbele katika utafiti kwa sababu ya uwepo wa machapisho haba kuhusu taaluma hii.

Kando na hayo, makala haya yamehusisha lugha mbili za Kibantu, Kiswahili na Lubukusu. Makala haya yameashiria Lubukusu kama lugha bali si lahaja ya Kiluhya kwa sababu ina sifa bayana zinazoitambulisha kama lugha (Lewis na wenzake, 2016;Watulo, 2018).Isitoshe, tafiti za awali zimebainisha kwamba lugha ya Lubukusu haijafanyiwa utafiti wa kutosha, hali inayoshadidiwa na uwepo wa machapisho machache katika lugha hii. Uchache wa machapisho unadhihirisha upungufu na mianya ya kufanya utafiti zaidi katika lugha hii ya Lubukusu (Nasambu, 2017). Kuna tafiti zingine ambazo zimependekeza kwamba pana haja ya kufanya utafiti zaidi katika lugha za kiasili.Tafiti hizi ni pamoja na Adicka (2016) alichunguza Kijaluo, Shidiavai (2015) Lwidakho, Owino (2016) alichunguza Kiwanga, Morara (2017) alitafiti Ekegusi na Muhammad (2017) alishughulikia Kiarabu, Kiswahili na Hausa. Usomaji wa tafiti zilizotajwa na upungufu wa maandishi katika Lubukusu na tawi la mofofonolojia ulimchochea mtafiti kuchunguza suala hili la utafiti.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

### Suala la Utafiti

Mada hii ilitokana na mapengo na mapendekezo yaliyodokezwa na tafiti za awali na ubainisho wa mtafiti kuwa hakuna tafiti mahsusi zinazorejelea kuathiriana kimofofonolojia kati ya lugha ya Kiswahili na Lubukusu kupitia ukopaji wa nominokutoka Kiswahili hadi Lubukusu hasa kwa kutumia misingi ya nadharia ya Mlingano Chanzi. Baadhi ya tafiti za awali ambazo zilidokeza mapengo yanayojalizwa na makala haya zinahusishwa na: Muambu(2014), Muandike(2011), Nasambu(2017), Lwangale (2018), Nandelenga (2013), Watulo (2018) na Nganga (2008).

### Malengo ya Utafiti

Makala haya yamekusudia kutimiza malengo yafuatayo:

- Kubainisha mifanyikombalimbali ya kifonolojia inayojitokeza katika nominomkopo kutoka lugha ya Kiswahili hadi Lubukusu.
- Kutambulisha mifanyiko mbalimbali ya kimofolojia inayojitokeza katika nominomkopo kutoka lugha ya Kiswahili hadi Lubukusu.
- Kutathmini ulinganifu wa muundo wa kimofofonolojia uliopo baina ya nominomkopo za Lubukusu na leksimu asilia za Kiswahili.

### Maswali ya Utafiti

Makala haya yamekusudia kujibu maswali yafuatayo:

- Je, ni mifanyiko ipi ya kifonolojia ambayo nominomkopo kutoka lugha ya Kiswahili hupitia kabla ya kusimilishwa katika muundo wa lugha ya Lubukusu?
- Je, ni mifanyiko ipi ya kimofolojia ambayo nominomkopo kutoka lugha ya Kiswahili hupitia kabla ya kusimilishwa katika muundo wa lugha ya Lubukusu?
- Je, kuna ulinganifu wowote wa kimofofonolojia baina ya nominomkopo za Lubukusu na leksimu asilia za Kiswahili?

### Sababu za Kuchagua Mada

Matokeo yamakala haya ya utafiti yatakuwa na umuhimu kwa makundi mbalimbali kama vile: kuongeza maarifa ya kiakademia kwa uwanja wa ukopaji na utafiti wa lugha za Kiasili, kuongeza hazina ya machapisho katika lugha ya Lubukusu ambayo inaonekana kuwa na machapisho machache, yatatumiwa kama marejeleo kwa watafiti katika taaluma ya fonolojia na mofolojia ya Lubukusu na Kiswahili na kuwasaidia watafsiri na watangazaji katika lugha ya Lubukusu na Kiswahili.

### Upeo na Mipaka

Makala haya yamechunguza vipengele vifuatavyo: matawi mawili ya kiisimu; fonolojia na mofolojia. Katika fonolojia yameshughulikia; fonimu, silabi, mkazo na toni ilhali katika mofolojia; mofimu, uambishaji, nomino na ngeli za nomino. Kadhalika, yameangazia sheria namabadiliko mbalimbali ya kifonolojia na kimofolojia yanayoongoza ukopaji wa nomino kutoka lugha ya Kiswahili hadi Lubukusu. Mwisho, aina ya maneno iliyoshughulikwa ni nominomkopo za Lubukusu kutoka Kiswahili.

## YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Dhana ya ukopaji wa kiisimu imeshughulikiwa na watafiti wengi awali lakini makala haya yametambulisha tafiti zinazoingiliana na utafiti huu au zinazodokeza mapengo ambayo mtafiti anakusudia kuyajaliza. Tafiti teule zimeainishwa kwa njia tatu: tafiti bayana kuhusu manenomkopo, tafiti za ukopaji kuhusu lahaja za Kiluhya na tafiti za ukopaji kuhusu Lubukusu.

### Tafiti Bayana Kuhusu Manenomkopo

Tafiti ambazo zimewasilishwa katika sehemu hii zimeshughulikia ukopaji katika lugha anuwai. Tafiti

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

hizo zinahusishwa na: Riro (2020) alitafiti kuhusu Kiingereza na Igikuria; Muhammad (2017) alichunguza Kiarabu, Kiswahili na Kihausa; Morara (2017) alichunguza Kiingereza naEkigusii; Uushona (2019) alitathmini Kijerumani na Oshiwambo; Adicka (2016) alichunguza Kiswahili na Kijaluo; Mutua (2013) Kikamba na Kiingereza; Muriira (2017) alichunguza Kiingereza na Kitigania; Gesare (2020) alichunguza Ekegusii; Cherotich (2017) alichunguza Kiswahili na Kikeiyo; Karuru (2013) alichunguza Kiswahili, Kiingereza na Gikuyu; Iribemwangi na Karuru (2012) walichunguza Kiswahili na Gikuyu; Tsangwa (2017) alichunguza Kiswahili,Kigiriamana Kikamba. Tafiti hizi zinachangia katika utafiti huu kupitiaubainishaji wa vikoa vya kisemantiki, mifanyiko ya kifonolojia na kimofolojia, mbinu za utafiti, miundo ya silabi na nadharia. Tofauti ni kwamba tafiti hizi zote zilishughulikia lugha tofauti, jamii lengwa tofauti na asilimia kubwa zilihusisha nadharia tofauti. Tofauti na mapengo yalioashiriwa katika tafiti hizo yanahalalisha mada hii ya utafiti.

### Tafiti za Ukopaji Kuhusu Lahaja za Kiluhya

Tafiti ambazo zimewasilishwa katika sehemu hii zinahusishwa na:Sasala na wenzake (2019) walichunguza Kinandi na Lukabarasi; Owino (2016) alichunguza Kiwanga; Shidiavai (2015) alichambua Kiswahili,Kiingereza na Lwidakho; Mukulo (2016) alichunguza Kiingereza na Lukabarasi. Tafiti hizi zinachangia utafiti huu kupitia dhana ya ukopaji katika lahaja mbalimbali za Kiluhya kwa sababu lugha ya Lubukusu ni mojawapo ya lahaja za Kiluhya. Ni wazi kwamba lahaja za Kiluhya zinatofautiana kimatamshi, uwekaji shadda na urefushaji wa vokali (Lwangale, 2018). Mwingiliano katika lahaja za Kiluhya umesaidia katika ubainishaji wa toni, silabi,fonimu, mbinu za utafiti, mifanyiko ya kifonolojia na kimofolojia na uchanganuzi wa data. Utofauti uliopo ulitenganisha utafiti huu na tafiti za awali kuhusu lahaja za Kiluhya.

### Tafiti za Ukopaji Kuhusu Lubukusu

Tafiti mbili zimewasilishwa katika sehemu hii. Kwanza, Muambu (2014) anayechunguza Kiingereza na Lubukusu na utafiti wake ulichangia utafiti huu kupitia utambuzi wa vikoa vya kisemantiki, michakato na sheria zinazoambatana na ukopaji wa maneno kimofofonolojia ilhali ulitofautiana na utafiti huu kupitia nadharia, lugha tafitiwa na mazingira ya ukusanyaji data. Pili, Muandike (2011) ambaye alichunguza lugha ya Kiingereza na Lubukusu. Utafiti wa Muandike ulichangia katika utafiti huu kupitia ubainishaji wa vikoa vya kisemantiki, jamii lengwa na aina ya maneno tafitiwa. Muandike, tofauti na utafiti huu alichunguza lugha ya Kiingereza na Lubukusu, tawi la mofolojia, nomino zilizoambatana na utamaduni mpya na alichanganua data kimaelezo na kihisabati.

Tafiti zilizowasilishwa zimedhihirisha kuwa watafiti wengi wameshughulikia taaluma ya ukopaji wa maneno katika lugha mbalimbali. Hata hivyo tafiti nyingi zilijikita katika ukopaji wa kifonolojia na kimofolojia na chache mno zilihusisha taaluma ya mofofonolojia kwa kutumia misingi ya nadharia ya Mlingano Chanzi. Kadhalika, hakuna utafiti mahsusi ambao ulichunguza nominomkopo kati ya lugha ya Kiswahili na Lubukusu hali ambayo imehalalisha mada hii ya utafiti.

## MISINGI YA NADHARIA

Makala haya yaliongozwa nanadharia ya Mlingano Chanzi ambayo inahusu maneno-mkopo na iliasisiwa na Smith (2009). Mkabala wenyewe ulibuniwa kutokana na mihimili ya Nadharia ya Upeo (Prince & Smolensky, 1993). Kando na hayo, Smith (keshatajwa) amependekeza mihimili miwili inayofanikisha utohozi wa maneno baina ya lugha shirikishi:

- Max – SB*(Maximal-SourceBorowing)* mhimili kuwa elementi za umbo la neno katika lugha changizi sharti zipatikane katika umbo la neno hilo katika lugha pokezi.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

- Dep – SB (*Dependent-SourceBorowing)* mhimili kuwa elementi za umbo la neno katika lugha pokezi sharti zipatikane katika umbo la neno hilo katika lugha changizi.

Mihimili hii iliongoza ulinganisho na ulinganuzi wa maumbo kati ya Kiswahili na Lubukusu, hali ambayo ilifanikisha uchanganuzi wa data katika makala haya.

## MBINU ZA UTAFITI

Data iliyotumika katika makala haya ilikusanywa kutoka maktabani na nyanjani. Maktabani kupitia usomaji wa vitabu, tasnifu, majarida na machapisho mengine yanayohusiana na mada hii ya utafiti. Pia, upekuzi wa maandishi mtandaoni ulinufaisha utafiti huu. Nyanjani; data ilikusanywa katika Kaunti Ndogo ya Kiminini, Kaunti ya Trans-Nzoia. Sampuli husika iliteuliwa kimaksudi na ilijumuisha wanawake 12 na wanaume 12 na wote walikuwa na umri kati ya miaka 30-50. Data ilikusanywa kupitia mahojiano ambayo yalihusu habari za kibinafsi na maswali mahsusi kutoka vikoa kumi na mbili vya kisemantiki. Vikoa hivyo ni; vifaa vya ujenzi, vyakula na vyombo vya nyumbani, teknolojia na mawasiliano, usalama na utawala, biashara na mavazi, siasa, elimu, dini, utabibu, gereji, sheria na ukulima. Walengwa wawili waliteuliwa kutoka kwa kila kikoa cha kisemantiki na takriban nominomkopo 220 zilikusanywa. Uchanganuzi wa data ulianza na uorodheshaji wa nomino zilizokusanywa kutoka nyanjani na kuzitafutia visawe vya lugha changizi, Kiswahili. Hatua iliyofuata ilikuwa ni kuchunguza maumbo ya nomino hizo katika mazingira ya lugha changizi, Kiswahili na lugha pokezi, Lubukusu ili kubainisha mabadiliko ya kifonolojia na kimofolojia ambayo nomino hizo mkopo zilipitia kabla ya kusimilishwa katika sarufi ya Lubukusu.Baadaye data iliwasilishwa kimaelezo kupitia mihimili mikuu ya nadharia ya Mlingano Chanzi.

## Maoni Kuhusu Fonolojia na Mofolojia ya Lubukusu na Kiswahili

Makala haya yamechambua vipengele vya kifonolojia na kimofolojia katika lugha ya Lubukusu na Kiswahili ili kudhihirisha ulinganifu uliopo kati ya lugha hizi. Vipengele vya kifonolojia ni; fonimu, silabi, mkazo, na toni na vya kimofolojia ni; mofimu, uambishaji, aina za nomino na mpangilio wa ngeli za nomino.

### *Fonimu za Lubukusu naKiswahili*

### Vokali za Lubukusu na Kiswahili

Hizi ni lugha za Kibantu kwa hivyo zinamfanano wa vokali tano fupi ambazo ni: [a, ɛ, I, ɔ na u]. Vokali hizi zina sifa bainifu zifuatazo: /a/; ni vokali itamkiwayo katikati, ulimi ukiwa chini na mdomo umetandazwa, /ɛ/; ni vokali itamkiwayo mbele, ulimi ukiwa katikati na mdomo umetandazwa, /i/; ni vokali itamkiwayo mbele, ulimi ukiwa umeinuliwa juu na mdomo umetandazwa, /ɔ/; ni vokali itamkiwayo nyuma, ulimi ukiwa katikati na mdomo umeviringwa na /u/; ni vokali itamkiwayo nyuma, ulimi ukiwa umeinuliwa juu na mdomo umeviringwa (Nandelenga, 2013; Rosenberg, 2014; Sikuku, 2011; Msanjila na wenzake, 2007: 13-15; Habwe na Karanja, 2004:48-50; Mgullu, 1999: 66-67; Mwaliwa, 2014: 83-95). Hata hivyo ni vizuri kutambulisha kwamba lugha ya Lubukusu inatofautiana na Kiswahili katika idadi ya vokali kwa sababu Lubukusu kando na kuwa na vokali fupi tano, lugha hii ina vokali zingine refu tano ambazo ni: [a:, ɛ:, i:, ɔ: na u] (Nandelenga, 2013; Rosenberg, 2014 na Sikuku, 2011).

### Konsonanti za Lubukusu na Kiswahili

Lugha ya Lubukusu ina konsonanti ishirini (Nandelenga, 2013; Rosenberg, 2014 na Sikuku, 2011) ilhali lugha ya Kiswahili, hata kama kuna mkinzano wa kimawazo kuhusu idadi kamili ya konsonanti; Kiswahili sanifu huwa na konsonanti ishirini na tano (Msanjila na wenzake, 2007: 13-15; Habwe na Karanja, 2004:48-50; Obuchi na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

Mukhwana, 2010: 83; Mwaliwa, 2014: 83-95).Nandelenga (2013);Rosenberg, (2014) naSikuku (2011) wameainisha konsonanti za Lubukusu kama ifuatavyo: Vipasuo: /p/; ni kipasuo sighuna cha midomo; /t/ ni kipasuo sighuna cha ufizini;/č/ ni kipasuo hafifu cha kaakaa gumu; na /k/ ni kipasuo hafifu cha kaakaa laini. Vikwaruzo:/β/, kikwaruzo ghuna cha midomoni; /f/ni kikwaruzosighuna cha midomo na meno; /s/ nikikwaruzo hafifu cha ufizini; na /x/ ni kikwaruzo hafifu cha ufizini. Nazali: /m/ ninazali ghuna ya midomoni; /n/ ninazali ghuna ya ufizini;/ɲ/ ninazali ghuna ya kaakaa gumuna; /ŋ/ni nazali ghuna ya kaakaa laini. Nazalishi awali: /mb/ ninazalishi awali ghuna ya midomoni;/nd/ ni nazalishi awali ghuna ya ufizini; /ɲɟ/ ninazalishi awali ghuna ya kaakaa gumuna; /ŋg/ ninazalishi awali ghuna ya kaakaa laini. Likwidi:/l/ nikitambaza ghuna cha ufizini na /r/ ni kimadende ghuna cha ufizini.

Viyeyusho:/j/ ni kiyeyushoghuna cha kaakaa gumu na /w/ ni kiyeyusho ghuna cha midomoni.Isitoshe, Mwaliwa (2014:88-95),Obuchi na Mukhwana (2010: 67-70) wameainisha konsonanti za Kiswahili kama ifuatavyo:Vipasuo: /p/ ni kipasuo, sighuna cha mdomoni; /b/ ni kipasuo ghuna cha mdomoni; /t/ ni kipasuo sighuna cha ufizini; /d/ ni kipasuo ghuna cha ufizini; /k/ ni kipasuo sighuna cha kaakaa laini; na /g/ ni kipasuo ghuna cha kaakaa laini.Vikwaruzo: /f/ ni kikwaruzo sighuna cha midomo na meno; /v/ ni kikwaruzo ghuna cha midomo na meno; /s/ ni kikwaruzo sighunacha ufizini; /z/ ni kikwaruzo ghuna cha ufizini ; /θ/ ni kikwaruzo sighuna cha menoni; /ð/ ni kikwaruzo ghuna cha midomo na menoni; /ʃ/ ni kikwaruzo sighuna cha kaakaa gumu; /ɤ/ ni kikwaruzo ghuna cha kaakaa laini; na /h/ ni kikwaruzo sighuna cha koromeo. Nazali: /m/ ni nazali ghuna ya midomoni; /n/ ni nazali ghuna ya ufizini; /ɲ/ ninazali ghuna ya kaakaa gumu; na /ŋ/ ni nazali ghuna ya kaakaa laini. Kitambaza: /l/ ni kitambaza ghuna cha ufizini. Kimadende: /r/ ni kimadende ghuna cha ufizini.Viyeyusho: /j/ ni kiyeyusho ghuna cha kaakaa gumu na /w/ ni kiyeyusho ghuna cha midomoni. Vizuiwa-kwaruzo: /č/ ni kizuiwa-kwaruzo hafifu cha kaakaa gumu na /ɟ/ ni kizuiwa-kwaruzo ghuna cha kaakaa gumu. Uainishaji wa konsonanti za Lubukusu na Kiswahili umeonyesha kwamba Lugha hizi zinamfanano wa konsonanti zifuatazo: [p, t, č, k, f, s, m, n, ɲ, ŋ, l, r, j na w] na zinatofautiana katika baadhi ya konsonanti:Kiswahili; [b, d, g, v, z, θ, ð, ʃ, ɤ, h na ɟ] na Lubukusu; [β, x, mb, nd, ɲɟ na ŋg].

**Silabi katika Lubukusu na Kiswahili**

Lugha zote za Kibantu hudhihirisha miundo mitatu ya silabi: konsonanti na vokali (KV), Vokali pekee (V) na Konsonanti pekee (K) (Nyabuto, 2015). Mawazo haya yameshuhudiwa katika lugha tafitiwa, Kiswahili na Lubukusu. Kiswahili na Lubukusu sawa na lugha ya Ekegusii, Lulogooli na Lwitakho huwa na silabi wazi (Ingonga, 1991; Morara, 2016). Lugha ya Lubukusu huwa na miundo minne ya silabi: konsonanti, konsonanti, vokali (KKV), konsonanti, vokali (KV), vokali (V) na nazali (N) (Nandelenga, 2013; Nganga, 2008). Kiswahili kando na kuwa na miundo mingine ya silabi, huwa na miundo minne mikuu ya silabi sawa na Lubukusu ambayo ni: konsonanti, konsonanti, vokali (KKV), konsonanti, vokali (KV), vokali (V) na konsonanti (K).Tofauti na dhana kwamba lugha ya Kiswahili na Lubukusu hudhihirisha mfumo wa silabi wazi, lugha ya Kiswahili pia husheheni mfumo wa silabi funge katika baadhi ya maneno hasa manenomkopo (Majariwa, 2021:113; Mwita, 2009:50; Okal, 2017:114).

**Toni katika Lubukusu na Kiswahili**

Machapisho mengi yamedhihirisha kwamba awali lugha zote za Kibantu zilikuwa lugha toni hata hivyo kutokana na mapito ya wakati baadhi ya lugha hizi zilipoteza sifa ya utoni na badala yake kusisitiza mkazo kama vile, Kiswahili na Kidigo (Kisseberth & Odden, 2003: 59; Downing, 2019: 75-76; Batibo, 2017: 35; Clements & Goldsmith, 1984:1). Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kwamba Kiswahili sio lugha toni bali Lubukusu ni lugha toni

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

na huwa na aina mbili kuu za toni;toni juu na toni chini (Nganga, 2008). Toni katika Lubukusu husaidia kubainisha maana ya maneno, njeo, dhamira, wakati na hali (Mutonyi, 1986).

## Mkazo katika Lubukusu na Kiswahili

Dhana ya uwekaji mkazo hutofautiana baina ya lugha kwa sababu kuna baadhi ya lugha ambazo sehemu ya kuwekamkazo hubadilika badilika ilhali lugha zingine haibadiliki(Mgullu, 1999:78).Kwa mfano katika Kiswahili na Lubukusu sawa na lugha zingine za Kibantu kama Kigiriama na Gikuyu mkazo huwekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho wa neno (Massamba, 2011: 218; Habwe & Karanja 2004:65; Msanjila na wenzake, 2007:28-29; Ngowa, 2008: 50; Waithaka, 2010: 48).

## *Ngeli za Lubukusu na Kiswahili*

Jedwali hili linaashiria Mpangilio wa ngeli katika Lubukusu na Kiswahili (Sikuku, 2011: 8; Mutonyi, 2000: 7-8; Rosenberg, 2014: 10-11; Obuchi & Mukhwana, 2010; Msanjila na wenzake, 2007; Habwe & Karanja, 2004; Mgullu, 1999).

**Jedwali 1: Mpangilio wa ngeli katika Lubukusu na Kiswahili**

| **Ngeli** | **Lubukusu (viambishi)** | | **Maoni** | **Kiswahili (viambishi)** | | **Maoni** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Umoja** | **wingi** | | **Umoja** | **wingi** | |
| 1-2 | **o-mw-** | **βa- βa-** | **o**-mw-ami – mtawala<br>**βa-βa**-ami- watawala | **mu-/mw-/m-** | **wa-** | **m**-tu- **wa**-tu<br>**mu**-uguzi –**wa**-uguzi |
| 3-4 | **ku-ku-** | **ki- mi-** | ku-mu-sa:la- mti<br>ki-mi-sa: la- miti | **mu-/mw-/m-** | **mi-** | **m**-ti- **mi**-ti<br>**m**-ungu- **mi**-ungu |
| 5-6 | li- li- | **ka- ma-** | **li:** -chuuma- wiki<br>**ka-ma**-chuuma- mawiki | **ji-/ ɸ-** | m**a-** | **ji**-tu- **ma**-jitu<br>**ji**-cho-**ma**-cho |
| **7-8** | **si- si-** | **βi- βi-** | **si:**faru – kifaru<br>**βi-** faru- vifaru | **ki-** | **vi-** | **ki**-ti- **vi**-ti<br>**ki**-su- **vi**-su |
| **9-10** | **e- n-** | **či- n-** | **e:** pu:si– paka<br>**či: -**pu:si– paka | **n- ɸ-** | **n- ɸ-** | nyama – nyama<br>kalamu- kalamu |
| **11** | **lu- lu** | **či-** | **lu-** βafu- ubavu<br>**či**-mbaafu- mbavu | **u -** | **n-** | **u**-devu- **n**-devu<br>**u**-jia- **n**-jia |
| **12-13** | **xa- xa-** | **-** | **xa-xa-** ana- mtoto mdogo<br>**xa-xa-** ala- kidole kidogo | **ka-** | **tu-** | **ka**-toto- **tu**-toto<br>**ka**-gari- **tu**-gari |
| **14** | **βu- βu-** | **-** | **βu**:-nya:si- nyasi<br>**βu**:-takha- umaskini | **u-** | **-** | **u**-tukufu- **u**-tukufu<br>**u**-zuri- **u**-zuri |
| **15** | **xu- xu-** | **-** | **xu:-**ka:la-kuzubaa<br>**xu:-** fwa-kufa | **ku-** | **-** | **ku**-cheza- **ku**-cheza<br>**ku**-imba- **ku**-imba |
| **16** | **a- na sya-** | **-** | **a:**-ndulo- kando<br>**sya**:-ndoo- karibu na ndoo | **pa-** | **-** | pale |
| **17** | **xu -** | **-** | **xu**:-nju- kwa nyumba | **ku-** | **-** | kule |
| **18** | **mu-** | **-** | **mu:-**ndoo- ndani ya ndoo | **mu-** | **-** | humu |

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

| Ngeli | Lubukusu (viambishi) | | Maoni | Kiswahili (viambishi) | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Umoja | wingi | | Umoja | wingi | |
| 20/4 | **ku-ku-** | **ki-mi-** | **ku-kwi**:-fwi – jizi<br>**ki-mi**:-fwi- majizi | - | - | |
| **23** | **e-** | **-** | **e-**βaa:na – upande wa watoto | | | |

Jedwali limetambulisha kwamba kimofolojia, lugha ya Kiswahili imegawanywa katika makundi 18 ya ngeli ambayo huwakilishwa na viambishi awali vifuatavyo: M-WA, M-MI, JI-MA, KI-VI, **N-/** ɸ, U/N, KA-TU, U, KU na PA-KU-MU na lugha ya Lubukusu ina viambishi ngeli 20: O-MU- / βA-Ba-, KU-MU-/KI-MI-, LI-LI -/ KA-MA-, SI-SI-/ βI-βI-, E-N-/ ČI-N-, LU-LU/ Či-, XA-XA-, BU-βU-, XU-XU-, A-/SYA-, XU-, MU-, KU-KU-/ KI-MI- na E-. Uchanganuzi wa makini wa viambishi hivi umebainisha kwamba baadhi ya viambishi ngeli hivi vinawakilisha makundi sawa ya viumbe, mimea au vitu lakini vinatofautiana katika maumbo katika lugha ya Lubukusu na Kiswahili.

***Aina za Nomino katika Lubukusu na Kiswahili***

Jedwali hili linaashiria aina za nomino katika Lubukusu na Kiswahili (Mutonyi, 2000; Ndalila, 2014; Obuchi na Mukhwana, 2010; Msanjila na wenzake, 2007; Mgullu, 1999).

**Jedwali 2: aina za nomino katika Lubukusu na Kiswahili**

| Lubukusu | Maoni | Kiswahili | Maoni |
|---|---|---|---|
| **Ukubwa** | Hutokana na uchopekaji wa kiambishi **ku-** kwa nomino zingine. Mfano; ku:saxulu- zee | **Pekee** | Hurejelea majina au vitu au mahali. Mfano; Nairobi. |
| **Udogo** | Hutokana na uchopekaji wa kiambishi**xa-** kwanomino zingine**.** Mfano;xa:saxulu- kizee | **Kawaida** | Hurejelea majina, vitu au mahali kupitia njia jumuishi.Mfano; wanyama |
| **Wingi** | Hudokeza hali ya wingi pekee hasa vimiminwa. Mfano; kame:chi- maji | **Wingi** | Hudokeza hali ya wingi pekee hasa vimiminwa. Mfano; maji |
| **Dhahania** | Nomino ambazo hazionekani, hazinusiki na hazionjeki. Mfano; βu:kesi- werevu | **Dhahania** | Nomino ambazo hazionekani, hazinusiki na hazionjeki. Mfano; ujinga |
| **Nomino Kopwa** | Hutokana na uchopekaji wa kiambishi**e-**kwanomino zingine**.** Mfano; e:njala- njaa | **Jamii** | Hutaja vitu au viumbe kupitia makundi mahsusi.Mfano; umati. |
| | | **Mguso** | Huashiria vitu vinavyoweza kushikika, kunusika, kusikika na kuonjeka. Mfano; ugali. |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

**Mabadiliko ya Kifonolojia na Kimofolojia katika Nominomkopo za Lubukusu kutoka Kiswahili.**

***Mabadiliko ya Kifonolojia***

Uchanganuzi wa data iliyokusanywa kutoka nyanjani umedhihirisha kwamba nomino zilizokopwa kutoka Kiswahili hupitia mabadiliko ya kifonolojia kama vile; ubadilishaji wa fonimu, uchopekaji wa fonimu, uyeyushaji wa vokali, urefushaji wa vokali, mabadiliko yanayohusu miundo ya silabi, uhifadhi wa konsonanti, uhifadhi wa mkazo na toni katika nominomkopo za Lubukusu.

***MabadilikoYanayohusu Fonimu***

**Ubadilishaji wa fonimu**

Ubadilishaji huu hutokana na utofauti wa kifonimu uliopo kati ya lugha chanzi na lugha pokezi (Mberia, 2004:46; Mndeme, 2019: 58; Adicka, 2016: 62; Mallya, 2018:79). Kwa mfano, katika lugha tafitiwa, yaani Kiswahili na Lubukusu, kadiri ilivyoelezwa hapo mwanzo ni bayana kwamba lugha hizi zinatofautiana sana katika mfumo na idadi ya fonimu. Hii ina maana kwamba nomino zinapokopwa kutoka Kiswahili hadi Lubukusu, nafasi ya fonimu za Kiswahili ambazo hazipatikani katika Lubukusu huchukuliwa na fonimu za Lubukusu ili kurahisisha matamshi na usimilishowa nomino hizo katika sarufi ya Lubukusu. Mifano ya fonimu za Kiswahili ambazo zilibadilishwa na za Lubukusu ni; /z/ ilibadilishwa na /s/, /b/ ilibadilishwa na /p/; /g/ ilibadilishwa na /k/. Hii ni kutokana na dhana kwamba fonimu /z/, /b/ na /g/ zinazopatikana katika Kiswahili hazipatikani katika Lubukusu ndiposazikabadilishwa na fominu /s/, /p/ na /k/ ili kufanikisha usimilsho wa kimatamshi na kimaumbo. Zingatia maneno yafuatayo pamoja na sheria ya mabadiliko ya kifonolojia:

| **Kiswahili** | **Lubukusu** |
|---|---|
| meza | e:me:sa |
| mbuzi | embusi |

/z/ ⟶ [s] / v-v

Sheria hii inaashiria kuwa fonimu /z/ hubadilika na kuwa /s/ katika mazingira ambayo inatokea katikati mwa vokali mbili.

**Udondoshaji wa Fonimu**

Udondoshaji hutokea pale ambapo fonimu hupotea katika mazingira fulani ya matumizi ya lugha mahsusi (Muambu, 2014:48; Obuchi & Mukhwana, 2010:88; Msigwa & Vavayo, 2020:40-41). Katika lugha tafitiwa, fonimu /h/ hudondoshwa katika nomino zinazokopwa kutoka lugha ya Kiswahili na kusimilishwa katika sarufi ya Lubukusu kwa sababu fonimu /h/ si mojawapo ya fonimu za Lubukusu. Hali hii imedhihirika katika nomino zifuatazo pamoja na sheria husika:

| **Kiswahili** | **Lubukusu** |
|---|---|
| kahawa | eka:wa |
| sahani | esa:ani |

/h/ ⟶ [ɸ] / -v

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

Sheria hii inadokeza kwamba fonimu /h/ hudondoshwa katika mazingira ya nominomkopo hasa inapotokea kabla ya vokali au kufuatwa na vokali. Hii nikwa sababu katika mazingira haya kutamka vokali huwa rahisi sana kuliko kutamka fonimu /h/ isiyopatikana mazingira ya lugha pokezi, Lubukusu.

**Uchopekaji wa Fonimu**

Kimsingi uchopekaji unaweza kuwa wa mwanzo, kati au mwishoni mwa neno (Mndeme, 2019: 48; Garoma, 2012:123). Kutokana na nomino ambazo zimekopwa kutoka Kiswahili hadi Lubukusu imebainika kwamba kuna uchopekaji wa vokali/u/ na /i/; konsonanti /l/ na /β/ (Muambu, 2014:50). Uchopekaji huu hutokea ili kubadilisha muundo wa silabi ya konsonanti pekee (K) hadi Konsonanti na vokali (KV), muundo ambao unakubalika katika Lubukusu.

Mifano ya vokali /u/ kutokana na data iliyokusanywa kutoka nyanjani:

| **Kiswahili** | **Lubukusu** |
|---|---|
| mkate | kumukati |
| mkeka | kumukeeka |

[ɸ] → /u/ / m____k

Sheria hii inadokeza kwamba vokali **/u/** huchopekwa katikati ya nazali **/m/** ikifuatwa na fonimu zingine za konsonanti kama vile vipasuo na vikwaruzo. Hali hii husababisha kuvunjwa kwa mfuatano wa konsonanti katika nominomkopo kutoka Kiswahili ili ziingiliane na sarufi ya Lubukusu.

Mifano ya konsonanti /β/ kutokana na data iliyokusanywa kutoka nyanjani:

| **Kiswahili** | **Lubukusu** |
|---|---|
| kifua | siifuβa |
| nguo | enguβo |

[ɸ] → /β/ / u____a

Sheria hii inadhihirisha kwamba konsonanti /β/ huchopekwa katikati mwa vokali /u/ na /a/ za nominomkopo ambazo zimekopwa kutoka Kiswahili hadi Lubukusu ili kuruhusu ukubalifu wa nomino hizo katika sarufi ya Lubukusu.

**Uyeyushaji wa Vokali**

Mabadiliko ya uyeyushaji hutokea wakati ambapo vokali za juu; /i/ na /u/ huchukua sifa za viyeyusho katika mazingira ambayo zinafuatana na vokali zisizofanana nazo. Muktadha wa utokeaji wa mabadiliko ya uyeyushaji hutegemea fonimu inayofuata vokali ambayo inayeyushwa bali sio fonimu inayotangulia vokali hiyo (Habwe &Karanja, 2004:62-63; Mashauri, 2021: 25). Dhana hii imeshuhudiwa katika baadhi ya maumbo ya nominomkopo za Lubukusu ambazo zilikusanywa kutoka nyanjani na zimedhihirisha uyeyushaji wa vokali /u/ hadi /w/, vokali /i/ hadi /j/ na sheria inayohusika:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

Mifano ya uyeyushaji wa vokali /u/ hadi /w/

| Kiswahili | Lubukusu | | |
|---|---|---|---|
| ngurue | [e:gurue] | → | e:ngurwe |
| miwa | [kumuiβa] | → | kumwiiβa |

/u/ → [w] / -v

Sheria hii inaeleza kwamba vokali ya nyuma, juu viringe /u/ hubadilika na kuwa kiyeyusho, ghuna cha midomoni /w/ katika mazingira ya kutangulia vokali [a, ɛ, I na ɔ].

Mifano ya uyeyushaji wa vokali /i/ hadi /j/

| Kiswahili | Lubukusu | | |
|---|---|---|---|
| gia | [e:kia] | → | e:kja |
| kofia | [e:kofia] | → | e:kofja |

/i/ → [j] / -v

Sheria hii inadokeza kwamba vokali ya mbele, juu tandaze /i/ hubadilika na kuwa kiyeyusho, ghuna cha kaakaa gumu /j/ katika mazingira ya kutanguliwa na vokali; [a, ɛ, ɔ na u].

**Urefushaji wa Vokali**

Mabadiliko haya husababishwa na utofauti wa kivokali kati ya Lubukusu na Kiswahili. Kiswahili kina vokali; [a, ɛ, I, ɔ na u]  na Lubukusu vokali kumi; fupi tano,  [a, ɛ, I, ɔ na u] na refu tano, [a:, ɛ:, i:, ɔ: na u]. Hivyo basi nominokopwa kutoka Kiswahili hupitia mabadiliko ya urefushaji wa vokali kabla ya kusimilishwa katika Lubukusu. Urefushaji wa vokali huambatana na mabadiliko mengine ya kifonolojia kama vile; muungano wa irabu, udondoshaji wa konsonanti na uyeyushaji.Kadhalika, urefushaji husaidia katika uongezaji wa wakaa wakati wa matamshi (Mashauri, 2021:37).

Mifano ya urefushaji wa vokali unaosababishwa na udondoshaji wa konsonanti inaonyeshwa kama ifuatavyo:

| **Kiswahili** | **Lubukusu** |
|---|---|
| kahawa | eka:wa |
| sahani | esaa:ni |

Mifano ya urefushaji wa vokali unaosababishwa na uyeyushaji wa konsonanti inaonyeshwa kama ifuatavyo:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

| **Kiswahili** | **Lubukusu** |
|---|---|
| Miwa | kumwi:βa |
| Moyo | kumwo:yo |

$I \longrightarrow [I:]_{fidia}$ / muungano wa irabu, udondoshaji au uyeyushaji

Sheria hii inaeleza kwamba vokali inayoambatana na nominokopwa kutoka Kiswahili hufanyiwa mabadiliko ya kifonolojia hasa kupitia urefushwaji na kuongezewa wakaa wakati wa utamkaji ili kufidia vokali iliyopotea aidha kupitia muungano wa irabu, udondoshaji au uyeyushaji ili ikubaliane na sarufi ya lugha pokezi, Lubukusu.

**Mabadiliko Inayohusu Miundo ya Silabi**

Ni bayana kwamba lugha tafitiwa Kiswahili na Lubukusu, zinaingiliana na kutofautiana katika miundo ya silabi. Utofauti katika miundo ya silabi hutokana na dhana kwamba lugha ya Lubukusu hairuhusu muundo wa silabi ya konsonanti pekee katika maumbo yake ya maneno. Ili kufidia udhaifu huu katika nominomkopo za Lubukusu kutoka Kiswahili, Lubukusu huruhusu uchopekaji wa vokali katikati mwa konsonanti fuatani. Muundo huu huashiria silabi wazi na hufanya nominokopwa kuingiliana kimaumbo na kimatamshi na lugha pokezi, Lubukusu (Kandagor & Sawe, 2014:112; Owino, 2003:133; Tasmia, 2016: 66-69; Mwita, 2009; 51).

Mifano ya uchopekaji wa vokali /u/ ili kuvunja mfuatano wa konsonanti katika nominomkopo kutoka Kiswahili hadi Lubukusu kama ifuatavyo:

| **Kiswahili** | **Lubukusu** |
|---|---|
| #**m**$ka$te# | #ku$m**u**$ka$ti# |
| #**m**$ke$ka# | #ku$m**u**$ke: $ka# |

$K$ ⟶ $KV$

Sheria hii inadokeza kwamba muundo wa silabi ya konsonanti pekee (K) katika mazingira ya Kiswahili, ambayo ni nazali umebadilika na kuwa konsonanti na vokali (KV) katika mazingira ya Lubukusu.

Mifano ya uchopekaji wa vokali /i/ ili kuvunja mfuatano wa konsonanti katika nominomkopo kutoka Kiswahili hadi Lubukusu kama ifuatavyo:

| **Kiswahili** | **Lubukusu** |
|---|---|
| #**spa**$na# | #s**i**$pa$na# |
| #**sp**i$ka# | #s**i**$pi$ka# |

$KKV$ ⟶ $KV$

Sheria hii inadokeza kwamba muundo wa silabi ya konsonanti, konsonanti na vokali (KKV) katika mazingira ya Kiswahili umebadilika na kuwa konsonanti na vokali (KV) katika mazingira ya Lubukusu.

**Uhifadhi wa Konsonanti**

Kadiri ilivyoelezwa hapo awali, ni wazi kwamba Kiswahili kinafanana na Lubukusu katika baadhi ya konsonanti nazo ni; [p, t, k, f, s, m, n, ɲ, ŋ, l, r, č, j na w]. Mfanano huu wa konsonanti husaidia katika

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

uhifadhi wa konsonanti wakati maumbo ya nomino huhamishwa kutoka Kiswahili hadi Lubukusu. Dhana hii imebainishwa kupitia konsonanti /p/ katika data iliyokusanywa kutoka nyanjanikama ifuatavyo:

| **Kiswahili** | **Lubukusu** |
|---|---|
| kipini | si: pini |
| paipu | epa:ipu |

Konsonanti zingine ambazo zilidhihirikakuhifadhiwa baina ya Kiswahili na Lubukusu kutoka kwa data iliyokusanywa kutoka nyanjani ni; [k, s, t, m, n, f, d na r]. Kadhalika, hakuna sheria teule ya kuashiria uhifadhi wa fonimu baina ya lugha hizi kwa sababu fonimu ambazo zimehifadhiwa zinapatikana katika Kiswahili na Lubukusu na fonimu hifadhiwa hutokea katika muktadha wowote katika maumbo ya nominokopwa baina yazo.

**Uhifadhi wa Mkazo**

Kimsingi, lugha ya Kiswahili na Lubukusu huwa na mkazo funge kumaanisha kwamba silabi inayowekwa mkazo haibadiliki bali husalia kuwa silabi ya pili kutoka mwisho wa neno (Ngowa, 2008: 50; Massamba, 2011: 218;Waithaka, 2010: 48). Mifano kutoka kwa data iliyokusanywa kutoka nyanjani ni kama ifuatavyo:

| **Kiswahili** | **Lubukusu** |
|---|---|
| ′nyama | e:′nyama |
| ′nyungu | e′nyu:ngu |

$$\sigma \longrightarrow [+\text{mkazo}] \,/\, -\sigma\ \#$$

Sheria hii inadokeza kuwa katika lugha ya Kiswahili na Lubukusu, mkazo huchopekwa kwa silabi ya pili kutoka mwisho wa neno.

**Toni katika Nominomkopo za Lubukusu**

Data kutoka nyanjani na udurusu wa maktabani umedhihirisha kwamba toni katika nomino za Lubukusu huwa ni kiambajengo cha mzizi wa nomino pamoja na viambishi awali; kwa sababu uwepo wa kiambishi awali katika nomino za Lubukusu huashiria toni juu. Isitoshe, ukopaji wa nomino kutoka Kiswahili umebainisha kwamba nominokopwahuambatana na mfumo wa mkazo ambao unaingiliana na mfumo wa toni katika Lubukusu. Hii ni kwa sababu silabi kaze pia huwa na nguvumsikiko zaidi wakati wa matamshi na huwa silabi toni pia hata kama kuna silabi zingine ambazo hubeba toni katika nomino rejelewa (Hyman, 2017; Marlo na wenzake, 2008; Marlo na Kristopher, 2015; Bwayo, 2011:11-12). Dhana hii imejitokeza katika nominomkopo zilizokusanywa kutoka nyanjani kama ifuatavyo:

| **Kiswahili** | **Lubukusu** |
|---|---|
| kitambaa | sí:[ta:mbáa] |
| sabuni | é[sabú:ni] |

***Mabadiliko ya Kimofolojia***

Msingi wa mabadiliko ya kimofolojia baina ya Lubukusu na Kiswahili ni utofauti wa viambishi ngeli kwa sababu lugha ya Kiswahili imegawanywa katika makundi 18 ya ngeli ambayo huwakilishwa na viambishi awali vifuatavyo: M-WA, M-MI, JI-MA, KI-VI, **N-/** ɸ, U/N, KA-TU, U, KU na PA-KU-

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

MU (Msanjila na wenzake, 2007:96; Habwe & Karanja, 2004:83-90) na lugha ya Lubukusu ina viambishi ngeli 20: O-MU- / βA-βA-, KU-MU-/KI-MI-, LI-LI -/ KA-MA-, SI-SI-/ βI-βI-, E-N-/ ČI-N-, LU-LU/ Či-, XA-XA-, BU-βU-, XU-XU-, A-/SYA-, XU-, MU-, KU-KU-/ KI-MI- na E- (Mutonyi, 2000:8-29; Rosenberg, 2014: 10). Uchanganuzi wa makini wa viambishi hivi umebainisha kwamba baadhi ya viambishi ngeli hivi vinawakilisha makundi sawa ya viumbe, mimea au vitu lakini vinatofautiana katika maumbo katika lugha ya Lubukusu na Kiswahili. Utofauti wa maumbo ya viambishi ngeli ndiyo husababisha mabadiliko ya kimofolojia wakati nomino huhamishwa kutoka Kiswahili hadi Lubukusu. Mawazo haya yanaingiliana na ya Karuru (2013: 7-10) aliyechunguza ukopaji wa maneno kutoka Kiswahili na Kiingereza hadi Gikuyu, na Morara (2017) alichunguza mofofonolojia ya nominomkopo kutoka Kiingereza hadi Ekigusii. Baadhi ya mabadiliko ambayo hutokea ni; ubadilishaji wa viambishi awali na uambishaji.

### *Ubadilishaji wa Viambishi*

Ubadilishaji wa viambishi awali umetokana na utofauti wa viambishi ngeli kati ya lugha Kiswahili na Lubukusu. Kwa mfano kiambishi /ki/ cha umoja katika mazingira ya Kiswahili hubadilishwa na kuwa kiambishi /si/ katika mazingira ya Lubukusu. Kadhalika, kiambishi /vi/ cha wingi katika Kiswahili hubadilishwa na kiambishi /βi/ cha wingi katika Lubukusu kama ifuatavyo kutokana na data iliokusanywa kutoka nyanjani:

| **Kiswahili** | | **Lubukusu** | |
|---|---|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** | **Umoja** | **Wingi** |
| ki [kombe] | vi [kombe] | si: [ko:mbe] | βi: [ko:mbe] |
| ki [tambaa] | vi [tambaa] | si: [taamba:a] | βi: [taamba:a] |

Katika mazingira mengine kiambishi awali cha umoja hurejelewa kwa mofu 62appa /ɸ-/ na wingi huchukua kiambishi /ma-/ katika mazingira ya Kiswahili. Viambishi hivi hubadilishwa na kiambishi kinominishi /li-/ katika umoja na viambishi /ka-ma-/ vya wingi katika Lubukusu kama ifuatavyo kutokana na data iliokusanywa kutoka nyanjani:

| **Kiswahili** | | **Lubukusu** | |
|---|---|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** | **Umoja** | **Wingi** |
| ɸ [sanduku] | ma[sanduku] | li: [sa:nduku] | kama[sa:nduku] |
| ɸ [blanketi] | ma[blanketi] | li: [ru:nge:ti] | kama[ru:nge:ti] |

Kadhalika, katika mazingira tofauti kiambishi awali cha umoja /m-/, /mu-/ au /mw-/ na /wa/ cha wingi katika Kiswahili hubadilishwa na viambishi vinominishi /o-mu/ au /o-mw-/ vya umoja na /βa-βa-/ vya wingi katika Lubukusu. Kwa mfano:

| **Kiswahili** | | **Lubukusu** | |
|---|---|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** | **Umoja** | **Wingi** |
| m[zazi] | wa[zazi] | omu:[sa:si] | βa:[sa:si] |
| mw[anafunzi] | w[anafunzi] | omw[anafunzi] | βaβa[anafunzi] |

### *Uambishaji*

Kutokana na data iliyokusanywa kutoka nyanjani ni wazi kwamba baadhi ya nomino kutoka Kiswahili, huchopekwa kiambishi ngeli katika mazingira ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

Lubukusu, ili zikubaliane na mfumo wa matamshi na maumbo ya maneno ya Lubukusu. Isitoshe, baadhi ya nomino ambazo huwa na kiambishi /m/ cha umoja katika mazingira ya Kiswahili hubadilika na kuchukua kiambishi ngeli /ku-mu/ cha umoja katika mazingira hayo katika Lubukusu na kiambishi /mi/ cha wingi katika Kiswahili huchukua viambishi /ki-mi/ vya wingi katika mazingira ya Lubukusu kama inavyoonekana katika mfano ufuatao:

| **Kiswahili** | | **Lubukusu** | |
|---|---|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** | **Umoja** | **Wingi** |
| m[kebe] | mi[kebe] | kumu[kepe] | kimi[kepe] |
| m[lango] | mi[lango] | kumu[lya:ngo] | kimi[lya:ngo] |

Katika mazingira mengine kiambishi awali cha umoja na wingi ambacho huashiriwa kwa mofu kapa /ɸ-/ katika mazingira ya Kiswahili hubadilishwa na kuwa kiambishi kinominishi kiashiria /e-/ katika umoja na /či-/ cha wingi katika Lubukusu kama ifuatavyo kutokana na data iliyokusanywa kutoka nyanjani:

| **Kiswahili** | | **Lubukusu** | |
|---|---|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** | **Umoja** | **Wingi** |
| ɸ[chokaa] | ɸ[chokaa] | e[choka] | či[choka] |
| ɸ [barua] | ɸ [barua] | e[barwa] | či [barwa] |

## HITIMISHO

Utafiti huu uligundua kwamba kuna mwingiliano na utofauti katika idadi ya fonimu kati ya Kiswahili na Lubukusu. Utofauti wa fonimu ndiyo msingi wa mabadiliko ya kifonolojia yanayotokea katika maumbo yanapokokotwa kutoka Kiswahili na kusimilishwa katika sarufi ya Lubukusu. Mabadiliko ambayo yametokanana mlingano na mlinganuo wa fonimu ni kama vile; ubadilishaji, udondoshaji, uchopekaji, uyeyushaji na urefushaji wa vokali. Mabadiliko mengine ambayo yameshughulikiwa ni uhifadhi wa konsonanti unaotokana na mfanano wa baadhi ya fonimu za konsonanti na mkazo.

Mkazo huwekwa kwa silabi ya pili kutoka mwisho wa neno katika nominomkopo za Lubukusu kutoka Kiswahili. Kadhalika, mabadiliko ya miundo ya silabi katika nominomkopo baina ya Kiswahili na Lubukusu yamechunguzwana kubainisha kwamba utofauti katika miundo ya silabi hutokana na hali ya lugha ya Kiswahili kuruhusu muundo wa silabi ambapo baadhi ya fonimu hasa nazali /m/ ambayo hubeba sifa ya usilabi na husimama kama silabi bila vokali dhana inayokubalika katika Kiswahili na haikubaliki katika Lubukusu. Mabadiliko mengine ya kifonolojia yaliyotambulishwa kupitia makala haya ni kipengele cha toni ambacho kimechambuliwa na uamuzi ukafikiwa kwamba Kiswahili sio lugha toni bali husisitiza mkazo ilhali Lubukusu huwa na mkazo na toni. Aidha, silabi kaze katika Kiswahili ndio mojawapo ya silabi ambazo huwekwa toni katika Lubukusu. Kadhalika, mabadiliko mawili ya kimofolojia ambayo nomino hizo hupitia yamewasilishwa. Kwanza, ni ubadilishaji wa viambishi awali; kwa kuzingatia kwamba lugha hizi mbili zina viambishi awali vya ngeli ambavyo vinatofautiana kwa hivyo wakati umbo la nomino hukokotwa kutoka Kiswahili huchopekwa kiambishi ngeli tofauti na kile cha awali kabla umbo hilo likubaliane na sarufi ya Lubukusu. Pili, ni mabadiliko yanayotokana na uambishaji wa viambishi awali. Katika haya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

mazingira umbo zima la nomino kutoka Kiswahili, huchopekwa kiambishi kinominishi awali ili umbo hilo liingiliane na sarufi ya Lubukusu. Mabadiliko haya yote huambatana na mihimili ya nadharia ya Mlingano Chanzi ambayo ndio msingi wa utafiti huu.

**Mapendekezo**

Utafiti huu umechunguza nominomkopo kutoka Kiswahili hadi Lubukusu kimofolojia na kifonolojia kwa msingi wa nadharia ya Mlingano Chanzi. Kwa hivyo kuna haja ya kufanya utafiti zaidi katika sehemu zingine kama vile; vitenzi kwa kuhusisha vipengele vya kifonolojia na kimofolojia. Uhusishaji wa matawi mengine ya kisimu kama sintaksia na pragmantikiunaweza pia kuendelezwa kupitia lugha zingine za Kibantuhasa lahaja za Kiluhya; na mwisho, imebainika kwamba lugha ya Lubukusu bado ina mawanda pana ya kufanyiwa utafiti kwa hivyo kuna haja ya kuendeleza utafiti huu kupitia misingi ya nadharia nyingine kama vile Nadharia Upeo au Fonolojia Zalishi Asilia.

**MAREJELEO**


Adicka, O.P. (2016). Utohozi wa Maneno-Mkopo katika lugha ya Kijaluo kutoka Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Batibo, H. M. (2017). Evolutionof Tone in Bantu Languages. *LiBRI. Linguistic and Literary Broad Research and Innovation*, *6*(2), pp. 34-40.

Bwayo, J. (2011).Open Source Spell Checker for Bukusu Dialect. Msc thesis. The University of Nairobi.

Cherotich, K.P. (2017). Fonolojia Arudhi ya nominomkopo kutoka Kiswahili hadi Kikeiyo.Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Clements, G. N., & Goldsmith, J. A. (1984). Auto-segmental Studies in Bantu Tone. Dordrecht: Foris Publications.

Downing, L.J. (2019). Tumbuka prosody: Between tone and stress. In Emily Clem, Peter Jenks & Hannah Sande (eds.), *Theory and description in African Linguistics: Selected papers from the 47th Annual Conference on African Linguistics*, 75–94. Berlin: Language Science Press.

Garoma, E. T. (2012). Phonology of Yem: Phonological processes. *Journal of Language & Culture*, 3(6), pp. 117-125

Gesare, E. M. (2020). A Morphophonological Analysis of Ekegusii Borrowed Segments. Ph.D dissertation. Kenyatta University.

Habwe, J.H., &Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Hyman, L.M. (2017). Bantu Tone Overview.University of California, Berkeley.

Ingonga, L. 1. (1991). A comparative study of Ekegusii, Lulogooli and Lwitakho. MA thesis. Kenyatta University.

Iribemwangi, P. I, Mbatiah, M. na Michira, N. (2013). *Ukuzaji wa Kiswahili: Dhima na Majukumu ya Asasi Mbalimbali*. Nairobi: Focus.

Iribemwangi, P. I., & Karuru, D. W. (2012). Phonological Adaptation of Kiswahili Loanwords in Gĩ-Gĩchũgũ Dialect of Gĩkũyũ Language. *Baraton Interdisciplinary Research Journal (BIRJ)* ,2 (2), 49-62.

Kandagor, M. & Sawe, S. (2014). Resyllabification of Loan Words in Kalenjin Phonology. Researchon Humanities and Social Sciences , 4(6).

Karuru, W. (2013). Borrowing and Communication in Language. *International Journal of Education and Research*, 1(9).

Kisseberth, C. W. & Odden, D. (2003). Tone. In Derek Nurse & Ǵrard Philippson (eds.), *The*

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

*Bantu languages*, 1stedn, 59-70. London: Routledge.

Lewis, M., Charles, D.F., Simons, & Paul, G. F. (2016). *Ethnoloque: languages of the world (*19thed). Dallas: SIL International.

Lwangale, D.W. (2018). Genealogical Reconstruction of the Proto-luhyia language. Ph.D Dissertation. Egerton University.

Majariwa, D. (2021). “Ukubalifu wa Silabi Funge katika Fonolojia ya Kiswahili.” Mwanga wa Lugha, 6(2) kur. 113-128.

Mallya, J.G. (2018). Phonological Processes in Chagga Nativized Lexemes Borrowed from Standard Swahili. M.A Thesis. Sanata Dharma University.

Marlo, M. R., & Kristopher J. E. (2015) Bukusutonology.MidPhon 20.Indiana University.

Mashauri, M. A. (2021). Upitiaji Upya wa Michakato ya Kifonolojia na Kanuni zake katika Kiswahili Sanifu. Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.19(1). 23-39.

Massamba, D.P. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Massamba, D.P.B (2011). *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia* .Dar es Salaam: TATAKI

Mberia, K. (2004). The Phonology of Borrowed Words in Kitharaka. Occasional Papers in Language and Linguistics, 2, 45-57.

Mesthrie, R., Leap, W. L., Deumert, A., & Swann, J. (2000). *Introducing Sociolinguistics*. Edinburgh: Edinburgh University Press.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mndeme, A. S. (2019). Phonological Processes of Shambaa. M.Athesis. St. Augustine University of Tanzania.

Morara, A. G. (2016). Syllabic Nativization of Ekegusii Loanwords From English: An Optimality Theory Approach. Elixir International Journal. *Literature 101 (2016) 44094 -44099.*

Morara, A. G. (2017). Phonological and Morphological Nativization of Ekegusii borrowed nouns from English. Ph.D Dissertation. Kisii University.

Msanjila, Y. P., Kihore, Y. M. na Massamba, D. P. B (2007). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (SAMAKISA). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Msigwa, A. G., & Vavayo, A. S. (2020). Dosari za Kifonolojia zinazojidhihirisha kwa Wajifunzaji wa Kiswahili katika Jamii ya Wamaasai. *Jarida la Chalufakita, Juz. Na. 2.*

Muambu, W. E. (2014). Morphophonological changesof Lubukusu borrowed words from English. *International Journal of English and Literature*, 5(2), 45-51.

Muandike, M. F. (2011). Cultural and Linguistic Borrowing of nouns from English to Lubukusu. M.A Thesis. Kenyatta University.

Muhammad, J.Y. (2017). A Morphophonological Analysis of Nouns Borrowed from Arabic in Hausa and Kiswahili. M.AThesis. Kenyatta University.

Mukulo, K.L. (2016). Phonological Analysis of Lukabarasi Loanwords from English. M.A Thesis. Moi University.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

Muriira, K. (2017). A Morphonological analysis of Loanwordsin Kitigania from English. M.A Thesis. Kenyatta University.

Mutonyi, N. (1986). A Morphological Study of the Affixation Process of Lubukusu. M. A Thesis. University of Nairobi.

Mutonyi, N. (2000). Bukusu morphology and phonology. Ph.D Dissertation. Ohio State University.

Mutua, N.B. (2013). The analysis of Kikamba Nativized Loanwords. M.A Thesis. Kenyatta University.

Mwaliwa, H. C. (2014). “An analysis of the syllable structure of standard Kiswahili loanwords from Modern Standard Arabic”. Ph.D.dissertation. The University of Nairobi.

Mwita, L.C. (2009). “The Adaptationof Kiswahili Loanwords from Arabic: A Constraint based Analysis”. *Journal of Pan-African Studies*, 2: 46-61.

Nandelenga, H. S. (2013). Constraint Interaction in the syllabic phonology of Lubukusu. Ph.D dissertation. Kenyatta University.

Nasambu, M.M. (2017). Lexical Variation in Lubukusu Spoken in Bungoma County. M.A Thesis. Kenyatta University.

Ndalila, H. K. (2014). Language Education as A Catalyst in Documenting Local Languages: a case of the lubukusu noun phrase. URI: http://ir.mu.ac.ke: 8080/xmlui/handle/ 123456789 /1913

Nganga, W.S. (2008). The tone structure of Lubukusu verbs and nouns. M.A thesis. Kenyatta University.

Ngowa, N. J.(2008). Mnyambuliko wa Vitenzi vya Kigiryama: Mtazamo wa Fonolojia Leksishi. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nyabuto, J. C. (2015) Phonological (A) Symmetries of Nasal Prefixesin Bantu. PhD dissertation. Michigan State University.

Obuchi, M. S., & Mukhwana, A. (2010). *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na vipengele*. Nairobi: A~Frame Publishers.

Okal, B.O. (2017). Uhakiki wa Fonimu na Miundo ya Silabi za Kiswahili. *African Online Journal volume* 13(1).

Owino, A.N. (2016). Mifanyiko ya Kimofofonolojia ya Ukuzaji na Udunishaji wa Nomino za Kiwanga. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Egerton.

Owino, D.(2003). Phonological Nativization of Dholuo Loanwords. Ph.D dissertation. University of Pretoria.

Prince, A., & Smolensky, P. (1993). *Optimality Theory: Constraint Interactionin Generative Grammar*. Malden, MA: Blackwell.

Riro, M. R. (2020). Linguistic Borrowing in a Language Contact Situation between Igikuria English. M.A Thesis. Kenyatta University.

Rosenberg, E. (2014). Lubuuya Noun Classes: Morphology and Semantic Affiliation. Gothenburg: University of Gothenburg.

Sasala, J. M., Mudogo, B. A., & Alati, R. A. (2019). Lexical Borrowing in Spoken Lukabaras in a Multilingual Context. *International Journal of Linguistics, Literature and Translation*, 2 (6), 31-37.

Shidiavai, M. (2015). A Phonological Analysis of Lwidakho Loanwords from Kiswahili and English. M.A thesis. University of Nairobi.

Sikuku, M. J. (2011). Syntactic Patterns of Anaphoric Relations in Lubukusu. Ph. D dissertation. The University of Nairobi.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1162

Smith, J.L. (2009). "Source Similarity in loan adaptation: correspondence theory and the posited source – Language representation" In *Steve Parker*, ed; Phonological. Argumentative Essay. On Evidence and Motivation. London. Equinox.

Tasmia, K. (2016). Isizulu Adoptives from English and Afrikaans. M.A thesis. University of the Witwatersrand.

Tsangwa, K.J. (2017). Ukopaji wa Maneno ya Kiswahili Sanifu Katika Kigiriama. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Pwani.

Uushona, J. (2019). An Investigation into the Phonological and Morphological Integrationof German Loanwords into Oshiwambo. M.A Thesis. The University of Namibia.

Waithaka, N. W. (2010). Mofolojia ya Manenomkopo ya Gikuyu kutoka Kiswahili.Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Watulo, A.W. (2018). The Inflectional Structure of Lubukusu Verbs. Ph.D Dissertation.Kenyatta University.

Wohlgemuth, J. (2009). *A Typology of Verbal Borrowings*. Berlin: Mouton de Gruyter. Tadmor.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.